



Hampton City Schools Administrative Center

ONE FRANKLIN STREET
Hampton, Virginia 23669-3570

Jeffery O. Smith, Ed.D.
Msimamizi wa Shule

Januari, 2022

Mpendwa Mzazi

Hampton City Schools itakuwa ikikubali maombi ya kitengo cha shule cha Choice Middle School Programu ya mwaka wa shule wa 2022-2023 kuanzia Jumatatu, tarehe 10 Januari, 2022. Fomu ya Maelezo ya Choice Middle School iliyoambatishwa inaangazia machaguo na kutangaza tarehe na saa za wazi kwa wote ili kukusaidia kufanya uamuvi wa ufahamu.

Ili kuhakikisha usawa katika uteuzi, viti vyta chaguo vitajazwa kupiti mfumo wa bahati nasibu. Wakati wa kutuma ombi la choice middle school, ni muhimu kuzingatia kwamba lazima mtoto na familia wawe tayari kujitahidi kwa mafanikio ya elimu na kuonyesha kujitolea kutimiza dhamira ya shule. Lazima familia zitoe usafiri kwa Mipango ya Choice Middle School.

Mchakato wa Ombi la Choice Middle School Application utapatikana mtandaoni kupitia tovuti ya Hampton City Schools kwenye <http://www.hampton.k12.va.us>. **Baada ya kukamilisha ombi mtandaoni, familia zitapokea thibitisho la wasilisho.** Lazima maombi yapokelewe kufikia Ijumaa, tarehe 11 Februari, 2022.

Taarifa kuhusu ukubalifu wa bahati nasibu kwenye Choice Middle School au uwekwaji kwenye orodha ya kusubiri zitatumwa kwa familia wiki ya tarehe 28 Februari, 2022. Katika barua pepe utapewa kiungo cha kuthibitisha uteuzi wako wa Choice Middle School bila kupitisha tarehe 18 Machi, 2022.

Pia wazazi wanaweza kuchagua kukamilisha ombi la Nje ya Kanda la shule ya kati kwa kuwasilisha ombi la Nje ya Kanda mtandaoni kwa mwalimu mkuu wa shule husika baada ya tarehe 28, Februari, 2022. Wazazi wataweza kukamilisha maombi ya Out-of-Zone mtandaoni kwenye tovuti yetu <http://www.hampton.k12.va.us>. **Uwekwaji kwenye nafasi za Out-of-Zone unalingana na upatikanaji na lazima wazazi** watoe usafiri. Wazazi wataarifwa kuhusu uwekwaji kwenye nafasi za Out-of-Zone kufikia tarehe 15 Agosti, 2022.

Tunakuhimiza uwasiliane na mwalimu mkuu wa shule yako au utembelee tovuti yetu kwenye <http://www.hampton.k12.va.us> ili kupitia maelezo kuhusu choice middle schools na ofa nyinyi za elimu ya ubora wa juu zilizopo katika Hampton City Schools.

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Jeffery O. Smith, Ed. D."

Jeffery O Smith, Ed. D.
Msimamizi

Viambatisho

Choice Middle School

MACHAGUO YA MPANGO

ANDREWS PREK-8

Wazi kwa Wote

Jumatano, tarehe 2 Februari,

2022

Saa 5:00-6:00 jioni



EATON FUNDAMENTAL

Wazi kwa Wote

Jumatano, tarehe Jumanne,

1 Februari 2022

Saa 6:30-7:30 jioni



JONES MAGNET

Wazi kwa Wote

Jumatano, tarehe Alhamisi,

3 Februari 2022

Saa 05:30-6:30 jioni



STEM Choice Program (Saa za Shule saa 9:00 asubuhi hadi saa 3:49 alasiri)

Hampton City Schools STEM Engineering Choice Program itawapa wanafunzi nafasi za kugundua kazi za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati. Mtaala huu wa mpango wa chaguo la kina wa miaka 3 umeundwa ili kuchochea na kuwapa wanafunzi changamoto kwa kujenga maarifa ya awali na stadi za kufikiria kwa kina. Wanafunzi watajifunza maagizo ya teknolojia ya kisasa pamoja na mafunzo ya muundo ili kuunganishwa na ulimwengu zaidi ya shule. Madarasa yatarejelea mada za kawaida za uhandisi kama vile: Utangulizi wa Uhandisi, Nyenzo na Mbinu za Uzalishaji, Uhandisi wa Muundo, Uhandisi wa Ufundii, Umeme na Elektroniki, Uhandisi wa Kemikali, Uhandisi Ujenzi na Uhandisi wa Tasnia. Lazima wanafunzi waonyeshe uwezo wa juu wa elimu. Ndugu wa wanafunzi walioeteuliwa katika darasa la-8 wataruhusiwa kuhudhuria Andrews kulingana na upatikanaji wa nafasi. Usafiri unatolewa kwa wanafunzi Waligawanywa KIKANDA pekee.

(Saa za Shule saa 9:00 asubuhi hadi saa

3:49 alasiri)

Thomas Eaton Middle School inawapa wanafunzi na familia zao hali ya elimu ya kina. Tuna matarajio makubwa ya wanafunzi wetu huku tukitoa mazingira yenye mpangilio na salama. Wanafunzi na wazazi wa Eaton wanatia sahihi kandarasi ya ushirikiano na shule, wakikubali kukamilisha mazoezi na kuonyesha tabia njema. Eaton inafanya vyema katika sanaa, shughuli za nje ya darasa, ushirikiano wa jamii, masomo ya huduma na hali za mazingira. Usafiri haupewi wanafunzi.

(Saa za Shule saa 8:49 asubuhi hadi saa

3:49 alasiri)

Jones Magnet Middle School (JMMS) ni shule bora ya mfumo wa kina. JMMS inatoa elimu ya ubora wa juu inayolenga ufanisi kwa kuangazia maagizo ya kina yanayojalizwa na shughuli muhimu huku ikianzisha mahusiano muhimu na wanafunzi. Uandikishaji ni wa kuitia mchakato wa kutuma ombi unaolingana na mfumo wa bahati nasibu. Usafiri haupo.

TAFADHALI FAHAMU MAKATAA

MAOMBI YANAHTAJIKA

KUFIKIA

**JUMATANO,
TAREHE IJUMAA,
11 FEBRUARI 2022**

**Maombi yanaweza
kukamilishwa kwenye:**
www.hampton.k12.va.us/choiceschools/choiceschools.html

